(4)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**


**MKOA WA DAR ES SALAAM**
**Anwani: "Afya"**
**Simu: +225-758 908110**
**Unapojibutafadhalitaja:**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA AMANA**
**S.L.P. 25411**
**DAR ES SALAAM.**


**17/12/2021**

**KUMB. NA. TRRH/F/28/17002**

# MKATABA WA UTOAJI HUDUMA YA UJENZI NA UKARABATI WA OPD NA EMD HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA AMANA.

Namba ya Mkataba: **ME/007/ARRH/2021-22/W/02**

Mkataba huu umefanyika leo tarehe **17 Mwezi 12 Mwaka, 2021**.

*KATI YA*

**MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA AMANA S.L.P 25411 DAR ES SALAAM ambaye** ni Mwajiri/ Afisa Masuhuli.

**JAPHET MIKAKALO** ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama mtoa huduma/Local Fundi kwa upande wa pili.

Kwa kuwa Mganga mfawidhi wa hospitali (Amana Hospital) anatarajia kufanya kazi ya **UJENZI NA UKARABATI WA OPD NA EMD HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA AMANA** ambapo chanzo cha fedha ni **SERIKALI KUU.**

Kama mtoa huduma/Local Fundi **JAPHET MIKAKALO** **nimekubali** kutoa huduma hiyo kwa muda wa siku 90 kuanzia tarehe nitakayokabidhiwa eneo la kazi.

**HIVYO PANDE ZOTE MBILI WANAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO;**

1. Kwamba Mkataba huu utakuwa ni wa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Tzs. **52,000,000** (million hamsini na mbili tu.), **ikiwa ni gharama za huduma ya Ujenzi na ukarabati wa OPD na EMD Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Amana.**
2. Utekelezaji wa **UJENZI** huu utafanyika mara moja na local fundi kwa kuzingatia ramani, ***"BOQ"*** na maelekezo yote yatakayotolewa na Mhandisi wa ujenzi kwa niaba ya Afisa masuhuli na kamati ya ujenzi.
   - Fundi atatakiwa kufanya kazi zote zinazohusika na kazi za ujenzi kwa awamu husika, ikiwa ni Pamoja na kufanya umwagiliaji wa maji katika zege, matofali, na kazi zinginezo.
3. Fundi atakuwa na wajibu wa kuweka mtaalamu au yeye mwenyewe kusimamia kazi za ujenzi wakati wote kazi zinaendelea eneo la ujenzi, na pia atatakiwa kufanya kazi kwa weledi na kuhakikisha anazingatia ubora na viwango vya kazi
4. Fundi wakati wote awapo eneo la kazi atapaswa kuzingatia sheria za nchi na kanuni za ujenzi ikiwa ni pamoja na kuwa na mavazi na vifaa vya kujikinga na ajali(protective gears)wakati wote fundi anapokuwa katika kazi za ujenzi
5. Kwamba mwajiri anaweza kusitisha mkataba huu wakati wowote endapo kutakuwa na kukiukwa kwa masharti ya mkataba.
6. Kwamba malipo yatafanyika kwa kuzingatia kazi zitakazo kaguliwa na karani na baada ya fundi kuwasilisha barua ya maombi ya malipo na Mhandisi kuhakiki kazi husika. **(Valuation of works)** na kutoa cheti ***"certificate"***
7. Kwamba mkataba huu utakuwa ni wa siku **90** kuanzia tarehe ya kukabidhiwa eneo la mradi.
8. Kwa makubaliano haya na masharti yote yaliyoainishwa na kukubaliwa na pande zote mbili yanakamilisha mkataba huu.
9. Fundi Mkuu atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha

mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.

10. Fundi Mkuu kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.

11. Fundi Mkuu atahusika na vitendo vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.

12. Fundi Mkuu kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.

13. Fundi Mkuu anatakiwa kuhakikisha anakuwepo muda wote eneo la ujenzi wakati kazi ikiendelea, Pia Fundi anatakiwa kupatikana muda wowote anapohitajika na uongozi wa Hospitali.

14. Fundi Mkuu anatakiwa kuwasilisha mpango kazi(SCOPE OF WORK) ambao unachanganua muda halisi wa kazi kuanza na kazi kumalizika kabla ya ujenzi kuanza.

15. Fundi Mkuu anatakiwa kuwasilisha Mchanganuo wa kazi kwa kila hatua ya ujenzi kulingana na muda wa ujenzi uliopangwa.

16. Fundi Mkuu anatakiwa kuhakikisha shughuli ya ujenzi inayoendelea haiathiri mifumo mingine ya Hospitali kama Umeme, Mfumo wa maji safi na maji taka na Mfumo wa TEHAMA au Shughuli nyingine yoyote ya hospitali.

- Ucheleweshaji wa Kazi:
  - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo..
  - Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri, Fundi ataomba aongezewe muda wa kumalizia kazi.

**NB: Mkataba huu unaweza kuvunjwa mara moja kwa mambo yafuatayo:**

- Iwapo fundi Mkuu au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Amana Hospitali.
- Iwapo Fundi Mkuu au Mafundi wake watafanya kazi bila kufuata mchoro au maelekezo ya Mhandisi Mshauri.

- Iwapo Fundi Mkuu au Mafundi wake hawatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake.

Iwapo Fundi Mkuu hatofika kazini siku tatu (3) mfululizo bila ya taarifa ya Maandishi.

**MKATABA UNASAINIWA NA KUWEKWA MUHURI WA MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA AMANA:**

**Jina** DR BRYCESON JOTT KIWELU

**Saini**

**Tarehe** 17/12/2021

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA AMANA
S. L. P. 25411
DAR ES SALAAM

**MBELE YA;**

**Jina :** ZAMZAM NDOSSI

**Sahihi ;**

**Cheo :** HOSPITAL ADMINISTRATOR

**KWA UPANDE WA MTOA (LOCAL FUNDI) HUDUMA**

**UMETIWA SAINI NA:**

**Jina** JAPHET PHILIPO MIKAKALO

**Saini** J. Philipo

**Tarehe** 17/12/2021

JAPHET PHILIPO MIKAKALO
P. O. Box 41587
DAR ES SALAAM

**MBELE YA**

**Jina** SIMON PHILIPO

**Saini**

**Tarehe** 17/12/2021